



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
MFUKO WA MISITU TANZANIA



MABADILIKO YA UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI YA RUZUKU

Mfuko wa Misitu Tanzania unatoa taarifa ya mabadiliko ya utaratibu wa kuwasilisha maandiko ya miradi kwa ajili ya kuomba ruzuku. Utaratibu wa awali ulikuwa na madirisha matatu ya kuwasilisha maandiko ya kuomba ruzuku. Madirisha hayo yalikuwa ni tarehe 31 Machi kila mwaka kwa maandiko yanayoomba ruzuku ya kati na kubwa, tarehe 30 Juni na tarehe 31 Desemba kila mwaka kwa maandiko yanayoomba ruzuku ndogo.

Kwa mujibu wa Kanuni za kusimamia utoaji ruzuku za mwaka 2021, umeweka utaratibu wa maandiko ya kuomba ruzuku ndogo, kati na kubwa kuwasilishwa **mara moja tu** kwa mwaka badala ya mara tatu. Aidha, tangazo la kuitisha maombi ya ruzuku litatolewa mwezi **Desemba kila mwaka** na mwisho wa kuwasilisha maandiko ya kuomba ruzuku ndogo, kati na kubwa utakuwa tarehe **31 Machi kila mwaka**.

Wenye nia ya kuomba ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Misitu Tanzania wanashauriwa kuzingatia utaratibu huu mpya na vilevile kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye Tangazo la kuitisha maombi ya ruzuku kwa mwaka husika.

Watakaohitaji ufafanuzi wanaweza kuwasiliana na Mfuko wa Misitu Tanzania kupitia anuani ifuatayo:

Katibu Tawala,
Mfuko wa Misitu Tanzania,

S.L.P. 1764, DODOMA.

Simu: +255 (0) 26 2963290, Nukushi: 255 (0) 26 2963290

Baruapepe: info@mfukowamisitu.go.tz Tovuti: www.mfukowamisitu.go.tz